

TAARIFA KWA UMMA

PENDEKEZO LA BEI YA NISHATI YA UMEME KUTOKA KWA WAZALISHAJI WADOGO WADOGO.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Madini na kwa kushirikiana na Benki ya Dunia wameweka mkakati wa kuharakisha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa watanzania wengi zaidi. Katika mkakati huo na kupitia shirika la TEDAP wadau hao wamejizatiti kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kuendeleza miradi ya umeme rejea yaani “renewable energy”. Ili kufikia malengo haya, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, imefungua wigo kwa wawekezaji binafsi kuwekeza katika miradi midogomidogo ya umeme.

Ili kufikia malengo haya, Wizara ya Nishati na Madini imetayarisha Mkataba wa Ununuzi wa Umeme yaani “Standardised Power Purchase Agreement” pamoja na mfumo wa kukokotoa bei yaani “Standardised Tariff Methodology”. Lengo la mkataba huu ni kuongeza uzalishaji wa umeme katika gridi ya taifa kupitia miradi midogo midogo. Pia Mkataba huu umelenga kuhakikisha kuwa maslahi ya wadau wote yanazingitiwa na kulindwa. Kulingana na kifungu cha 17 cha Sheria Na. 414, Mkataba pamoja na mfumo wa bei viliidhinishwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) mwaka 2008. Katika hali ya kawaida, Mfumo wa kukokotoa bei unapitiwa kila baada ya miaka mitano. Hata hivyo marekebisho yatokanayo na mwenendo wa mfumuko wa bei nchini hufanyika kila mwaka. Marekebisho hayo yanafanywa na kikosi kazi yaani “working Group”. Licha ya mfumo wa kukokotoa bei kutakiwa kufanyika kila baada ya miaka mitano, marekebisho ya sasa ilibidi yafanyike kabla ya kipindi hicho ili:- (a) kuondoa kipengele kinachohusu gridi ndogo kwenye mfumo wa kukokotoa bei ambacho kwa sasa kinajitegemea na (b) kutoa ufananuzi wa tafsiri kuwa kiwango cha umeme husika yaani Megawati 10 ni kile kitakachouzwa na mzalishaji ikiwa ni pamoja na umeme wa mabaki ya mazao viwandani yaani “cogeneration”.

Kila mwaka kikozi kazi chenye wajumbe kutoka Wizara ya Nishati na Madini, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, REA, Umoja wa Sekta binafsi nchini yaani “Tanzania Private Sector Foundation”, TANESCO na EWURA (kama mwangalizi) hukutana na kukokotoa bei ya nishati ya umeme kwa mwaka husika na kuwasilisha EWURA kwa maidhinisho. Kikozi kazi hicho kimepitia na kuwasilisha EWURA mambo yafuatayo:

- i. Marekebisho ya Mfumo wa Kukokotoa bei kwa wauzaji wa umeme kwenye Gridi kuu yaani “Main-Grid”;
- ii. Mfumo wa Kukokotoa bei kwa wauzaji wa umeme kwenye Gridi ndogo yaani “Mini grid”;

- iii. Kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali Na. 1 pendekezo la bei la uuzaji wa umeme kwenye Gridi kuu yaani “ Main-Grid” kwa mwaka 2009; na
- iv. Kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali Na. 2 pendekezo la bei la uuzaji wa umeme kwenye Gridi ndogo yaani “ Mini grid” kwa mwaka 2009;

Jedwali 1: Bei ya kuuzia umeme kwenye Gridi Kuu

Wastani wa bei ya Umeme kwa Wazalishaji Wadogo wadogo			85.49	TZS/kWh
Bei itabadilika kulingana na msimu	Msimu wa jua/kiangazi	Agosti – Novemba	102.58	TZS/kWh
	Msimu wa mvua/masika	Januari - Julai na Desemba	76.94	TZS/kWh

Jedwali 2: Bei ya kuuzia umeme kwenye Gridi Ndogo

Bei ya kuuzia umeme toka miradi midogo midogo kwa 2009	334.83	TZS/kWh
--	--------	---------

Ikumbukwe kuwa, Mikataba wa Ununuzi wa Umeme yaani SPPAs itakayosainiwa katika kipindi cha mwaka 2009, bei ya chini (floor price) itakuwa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali hapo juu na bei ya juu (price cap) itakuwa ni mara moja na nusu (1.5) ya bei, na bei itarekebisha ili kuendana na mfumuko wa bei nchini.

Kulingana na kifungu Na.19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, wadau wote wanakaribishwa kuwasilisha maoni yao, kwa maandishi au vinginenvyo, juu ya uhalali wa bei zilizotajwa hapo juu ndani ya kipindi cha wiki tatu (siku 21) tokea tarehe ya tangazo hili.

Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu wa EWURA.